*Pasaka na Ubatizo wa Wakatekumeni*

## Kuingizwa katika maisha ya Kristu

Wakatekumeni waliofanya Hatua ya Pili na wanajiandaa kupokea Ubatizo wakati wa Paska mwaka huu wametoka katika makanisa ya Ol Moran, Githima, Mithuri na Lounyek.

Kwa njia ya pekee, Paska ni wakati unaofaa kwa kupokea Sakramenti za Kuingizwa Ukristu, yaani Ubatizo, Kipaimara na Komunio Takatifu. Hasa Usiku wa Pasaka ni ibada Wakatekumeni wanapostahili kubatizwa, kwa sababu ni siku tunaposherehekea kufufuka kwake Kristu, yaani ukamilifu wa wokovu na mwanzo wa maisha mapya. Ubatizo ni mlango wa kuingia katika maisha mapya ya Kristu Mfufuka, na katika Kanisa lake.

Kwa sababu hiyo, katika Kesha ya Paska, vile vile katika ibada ya Jumapili zinazofuata, katika makanisa yetu kadhaa kutakuwa na Ubatizo wa Wakatekumeni wanaomaliza kujifunza Katekismu, na kwa njia ya Sakramenti hizi wataanza maisha ya Kikristu.

Ni vema Wakristu wote wawaombee Wakatekumeni wetu wakijiandaa kwa hatua hiyo muhimu.

*HABARI FUPI - HABARI FUPI - HABARI FUPI - HABARI FUPI*

### *Associations & Groups*

*- CMA*

Executive ya CMA ilikutana Jumamosi 8 Machi kupanga kazi za chama kwa mwaka 2014. Walipitisha pia kwamba mchango wa kujiandikisha mwaka huu utakuwa KShs 320 kwa wanachama, au KShs 380 kwa watu wapya.

Wanachama wote watatembelea kanisa la Mithuri Jumapili 30 Machi, baada ya Ibada. Tena, mwezi wa Aprili watatembelea kanisa la Kahuho. Bali mwezi wa Mei, Jumapili tarehe 5, watafanya Nadhiri zao katika ibada ya saa tano, Ol Moran.

*- CA*

Jumatano 2 Aprili, saa nne, kutakuwa na mkutano wa waakilishi wa Viongozi wa CA: kiongozi mmoja kutoka katika kila Kanisa, ili kujadiliana kuhusu mpango wa kazi za chama.

Wanachama wote watamtembelea bw. Joseph Njama nyumbani kwake, Minjore, Jumatano 16 Aprili, saa nne.

*- PMC*

Promoters wa PMC walikutana Jumamosi 22 Machi jioni, ili kupanga kazi mbalimbali za watoto.

Waakilishi wa watoto na wa Promoters (Wavulana 5, Wasichana 5 na Promoter 1) watahudhuria Semina itakayofanywa kwa ajili ya Jimbo lote, katika Parokia ya Ol Joro Orok, kuanzia Jumatano 23 hadi Jumamosi 26 Aprili. Malipo ni KShs 1,200 (Kujiandikisha na safari).

Pia, watoto wa PMC wameanza kujitayarisha kwa Mashindano ya Nyimbo katika makanisa. Mada ya mwaka huu ni: "Maria, kielelezo cha maisha yangu" ("Mary, my Role Model").

*- CHOIR: Semina ya Parish, na 'Singing Together'*

Wanakwaya walikutana mara kadhaa mwezi uliopita na mwanzoni mwa mwezi huu ili kujiandaa kwa sababu ya huduma ya Ibada ya Harambee.

Baadaye, Viongozi wa Kwaya walikutana Ijumaa 21 Machi ili kupanga kazi nyingine za mwaka huu. Semina ijayo itafanywa kuanzia Alhamisi 10, saa kumi, hadi Jumamosi 12 Aprili. Pia wanajiandaa kwa Semina ya Jimbo *"Singing Together"* itakayofanywa kwenye Shule ya Upili ya Leshau (Mutanga Parish), tarehe 20—26 Aprili 2014.

***Kalenda ya Machi-Aprili 2014***

***Main Activities and Sunday Gospels***

*Jumapili 30 Machi* - ya 4 ya Kwaresima - A - *(Yoh 9:1-41)*

*Jumamosi 5 Aprili*
→ Ol Moran, 7.00am: Hike ya Maskauti Rovers
→ Ol Moran, 10.00am: Mkutano wa Makatekista wote

*Jumapili 6 Aprili* - ya 5 ya Kwaresima - A - *(Yoh 11-1-45)*

*Alhamisi 10 (hadi Jumamosi 12 Aprili)*
→ Ol Moran, 4.00pm: Semina ya Kwaya

*Ijumaa 11 Aprili*
Mwisho wa Muhula wa 1 wa Shule

***JUMA KUU 2014***

*Jumapili 13 Aprili* - **JUMAPILI YA MATAWI**
*Kuingia Bwana Yerusalemu*
→ Ol Moran, 10.00am: Maandamano ya Matawi na Misa ya Mateso

*Alhamisi 17 Aprili* - **ALHAMISI KUU** - *Karamu ya Mwisho na Kutawadha Miguu - Mwanzo wa Upadrisho na wa Ekaristi Takatifu*
→ Nyahururu, 10.00am: Misa ya Kuyabariki Mafuta Matakatifu na Sherehe ya Mapadri wote wa Jimbo pamoja na Askofu
→ Ol Moran, 2.00pm: Semina ya Pasaka ya Vijana (hadi Jumapili 20)
→ Ol Moran, 4.00pm: Misa ya Karamu ya Mwisho na Kutawadha Miguu.
→ Ol Moran, 8.00pm: Kesha ya Kuabudu Ekaristi Takatifu.

*Ijumaa 18 Aprili* - **IJUMAA KUU** - *Mateso na Kifo cha Bwana - Siku ya Kufunga - Sadaka maalum ya Kaburi Takatifu*
→ Ol Moran, 3.00pm: Njia ya Msalaba na Ibada ya Mateso ya Bwana

*Jumamosi 19 Aprili* - **JUMAMOSI KUU** - *Kaburi la Bwana*
→ Ol Moran, 7.00pm: Kesha na Misa ya Pasaka (Ubatizo)

*Jumapili 20 Aprili* - **PASKA YA UFUFUKO** - *(Yoh 20:1-9)*
→ Magadi, 9.00am: Misa ya Pasaka
→ Ol Moran, 11.00am: Misa ya Pasaka

*(Misa na Ibada nyingine zitapangwa ikiwa tutapata msaada wa Mapadri wengine. Makanisa yatajulishwa baadaye).*

*Jumapili 20 Aprili (hadi Jumamosi 20 Aprili)*
→ Mutanga Parish, 4.00pm: Semina ya Kwaya "Singing Together"

*Jumatano 23 Aprili (hadi Jumamosi 20 Aprili)*
→ Ol Joro Orok Parish, 10.00am: Semina ya PMC

*Jumapili 27 Aprili* - ya 2 ya Paska - A - *(Yoh 20:19-31)*

*Ijumaa 2 Mei (hadi Jumamosi 3 Mei)*
→ Ol Moran, 7.00pm: Semina ya 2 ya Junior Catechists

*Jumamosi 3 Mei*
→ Ol Moran, 10.00am: Mkutano wa Makatekista wote

*Jumapili 4 Mei* - ya 3 ya Paska - A - *(Mt 5:13-16)*

*Jumatatu 5 Mei*
Mwanzo wa Muhula wa 2 (Hekima House na Tumani Academy)

**Ubatizo wa Watoto Wachanga:** 16 Feb: Miharati, Watoto 3; Kahuho 1; Ngare -Narok 8; Ol Moran (27) — 26 Feb: Kabati 8; Githima 12; Mithuri 4; Nagum 10 — 2 Mar: Mouarak 50 — 4 Mar: Dam Mbili 14.
**Mazishi ya Waumini:** Mary Wanjugu Mwangi, Peter Kamore Githaiga (Ol Moran, 29/03).

SAUTI *YA MTAKATIFU* MARKO
- No. 52, Year 6, Printed for private use at Ol Moran, Kenya, on 29th March 2014 -
**SAINT MARK** CATHOLIC PARISH - Ol Moran - *Catholic Diocese of Nyahururu*
*P.O.Box 20 - 20320 Kinamba* - saintmark@olmoran.it - *+254 720 924 153*

### Juma Kuu na Kipindi cha Paska 2014

Tumeendelea katika safari ya Kwaresima na sasa tunakaribia kiini cha mwaka wa Kanisa, yaani Juma Kuu na Sherehe ya Pasaka ya Bwana wetu Yesu Kristu.

**Juma Kuu** litaanza Jumapili ya Matawi, tarehe 13 Aprili.

**Siku Tatu Kuu** za Paska zitaanza Alhamisi Kuu jioni (17 Aprili), Ijumaa Kuu, Jumamosi Kuu, Jumapili ya Ufufuko (20 Aprili).

Jumapili ya Ufufuko ni mwanzo wa **Oktava ya Paska,** yaani siku nane ya Ufufuko (hadi Jumapili ya pili ya Paska, tarehe 27 Aprili), pia ni mwanzo wa **Kipindi cha Paska,** kinachodumu siku 50, hadi Jumapili ya Pentekoste (tarehe 8 Juni).

Katika ukurasa wa nne unapatikana utaratibu wa Ibada za Juma Kuu katika Parokia yetu.

### 2014: Mwaka wa Familia

Katika Sherehe ya Jimbo (22 Machi), Askofu Joseph alifungua rasmi **Mwaka Maalum wa Familia** kwa ajili ya Jimbo la Nyahururu. Nia ya Mwaka huu ni kutafakari zaidi kuhusu maadili ya familia ya Kikristu, na kuziombea familia zetu. Mwaka huu hata Maaskofu wa dunia katika Mkusanyiko Mkuu (*Synod of Bishops*) watajadiliana kuhusu changamoto za familia katika jamii ya kisasa.

*Vijana wa Parokia*

### Nadhiri za Mwaka na Semina ya Paska

**Mkutano wa Waakilishi -** Waakilishi wa Vijana kutoka kila Kanisa walikutana Jumamosi 29 Machi kupanga kazi za vikundi vyao.

**Music Festivals** - Mwaka huu mada ya Mashindano ya Vijana itakuwa kuhusu Mwaka wa Familia. Vijana wameanza kujiandaa.

**Maandamano ya Matawi na Nadhiri za Vijana -** Kama kila mwaka, Jumapili ya Matawi Vijana waliojiandikisha katika kikundi chao watafanya Nadhiri. Mwaka huu itakuwa Jumapili 13 Aprili. Vijana wote wa Parokia watahudhuria ibada Ol Moran, saa nne, kuanzia na Maandamano ya Matawi.

Ni jukumu la Vijana, pia, kutengeneza matawi ya Maandamano na nyimbo za ibada hiyo.

**Semina ya Siku Tatu Kuu za Paska -** Sherehe ya Paska ni ile Sherehe kubwa kuliko zote katika maisha ya Kanisa. Ili kusaidiana kuishi vizuri Siku Tatu Kuu za Paska na kuhudhuria pamoja ibada zao, Vijana watakuwa katika Semina kuanzia Alhamisi Kuu, tarehe 17 Aprili (saa kumi Misa ya Karamu ya Mwisho) hadi Jumapili ya Ufufuko, tarehe 20 Aprili.

SAUTI

*YA MTAKATIFU* MARKO

**Mt. Marko Mwinjili na Msimamizi wa Parokia**
*Aliishi Yerusalemu. Baada ya ubatizo wake, akafuatana na Mtume Paulo. Halafu aliishi Roma na Mt. Petro, akaandika Injili akikusanya mafundisho yake. Akaeneza Ukristu na kuanzisha Kanisa Aleksandria ya Misri. Kwa hivyo, alikuwa Mhubiri, Askofu na Shahidi wa kwanza kwenye bara la Afrika.*

**Gazeti la Parokia Katoliki ya Mtakatifu Marko Mwinjili ya Ol Moran**
*N. 52 — Mwaka wa 6*

**Machi 2014**

*Paska 2014*

# Asili ya Amani

Kuna wimbo mmoja wa zamani, unaoongea kuhusu siku ya Pasaka, unaosema:

*"Siku ya kwanza na ya mwisho,*
*Siku ya jua na mwangaza,*
*Siku ya ushindi wa Kristu.*

*Bwana Mfufuka*
*Atangaza milele*
*Sheria ya Amani.*

*Amani kati ya mbingu na nchi,*
*Amani baina ya Mataifa,*
*Amani moyoni mwetu".*

Ushindi wa Kristu katika mateso, kufa na kufufuka kwake ni amani. Siku ile ya kufufuka kwake, alipojionyesha hai kwa Mitume, Yesu aliwasalimu na maneno haya: "Amani iwe kwenu" (Yoh 20:19). Amani ni ile zawadi ya kwanza ya ushindi wake.

Kristu ameshinda juu ya fitina ya Shetani, juu ya chuki na uovu, juu ya utawala wa mauti. Ili tuwe na amani katika mapenzi ya Mungu.

Wakristu wapendwa, tunakaribia Sherehe ya Paska. Hiyo ndiyo Sherehe kubwa kuliko sherehe zote na kiini cha maisha ya Kanisa na ya kila Mkristu. Twadhimisha kifo chake Bwana Yesu na ufufuko wake. Maisha yote ya Kanisa yaanza na Kristu Mfufuka. Maisha yetu yaanza hapo. Yeye, Kristu, ni chemchemi ya maisha mapya, asili ya mema yote na mwanzo wa amani.


"Yeye ndiye amani yetu" (Ef 2:14). Paska ni sherehe ya amani: tujiandae kupokea tena amani kati yetu na Mungu: tukifanya kitubio, tukisikia Neno lake, tukitafuta mapenzi yake.

Kristu aliyekufa na kufufuka ni kiini cha imani ya Kanisa. Yeye ndiye amani yetu.

Tujenge tena amani na ndugu zetu, tukiwa na moyo wa ukarimu na huruma, hasa kwa walio na shida; tupatane tena na wale tuliotengana nao, au kunyamaziana. Tukubali amani ya Kristu itawale miongoni mwetu.

Nawatakia Paska njema!

Fr. Giacomo Basso - *Baba Paroko*



*Harambee ya Ujenzi wa Kanisa — 9 Machi 2014*

# Mashindano ya Ukarimu

MAANDALIZI — Kazi ya kuandaa Harambee ilianza miezi sita iliyopita, wakati katika Parish Assembly ya 9, Jumamosi 7 Septemba 2013, Viongozi walipoamua kuuchangia zaidi mradi wa Ujenzi wa Kanisa. Tangu wakati ule, kila familia yetu ilijaribu kutoa angalau gunia moja la mahindi, pia pesa kwa ajili ya kununua mabati ya kanisa. Wakristu wengi wamejaribu sana, na siku ya Harambee walileta mbele ya Askofu Luigi mazao ya kazi zao.

SIKU YENYEWE — Jumapili tarehe 9 Machi 2014, siku ya Harambee kwa ajili ya Ujenzi wa Kanisa, sherehe ilianza saa nne na ibada ya Misa iliyoongozwa na Askofu Mstaafu Luigi Paiaro, Mgeni Mkuu wa Harambee.

Wakristu na Wageni wengi walifika mapema. Mara moja baada ya ibada vikundi kadhaa waliimba nyimbo za kuburudisha, yaani: Tumaini Academy (Ngare-Narok), Ol Moran Peace Club, Good Shepeherd Minor Seminary (Maralal).

Harambee ilifunguliwa na mwaliko wa Baba Paroko kushiriki kwa ukarimu katika mchango. Halafu, Viongozi wa kila Kanisa la Parokia walileta michango ya makanisa na Wakristu wa Parokia, hasa matokeo ya mahindi na ya mabati. Halafu ulikuwa wakati wa wageni, marafiki, wafanyabiashara na wanasiasa waliohudhuria sherehe. Vikundi pia, shule kadhaa, vyama vya Parokia viliweza kuuchangia mradi.

Zaidi ya hayo, marafiki na wafadhili wengine walituma michango yao kwa benki au kwa M-Pesa. Hata kazi nyingine zilichangia, kama maua yaliyouzwa, au faida ya "Simba Kiosk".

Michango ya Harambee itasaidia kuendelea na kazi ya kujenga kanisa, ambayo si ndogo bado. Matokeo ya Harambee yaweza kusomwa katika *The Echo*.

KAMATI YA HARAMBEE — Jumatano 19 Machi Kamati ya Harambee ilikutana ili kutathmini kazi ilivyofanywa na matokeo ya michango.

Kamati inataka kuwashukuru sana Wakristu wote kwa bidii yao. Pia, Askofu Luigi, wageni, marafiki, wanasiasa na watu wa Serikali, watoto wa familia zetu na wote waliotaka kutusaidia katika mchango wa Harambee. Shukrani pia kwa wafanyakazi na wote waliosaidia kutengeneza siku ya Harambee.

Bila shaka, Harambee hii imekuwa siku nzuri ya sherehe na mshikamano, yenye fanaka, tena siku ya mashindano ya ukarimu.

Mbarikiwe zaidi!







Picha za Siku ya Harambee. Picha ya katikati: Mgeni Mkuu Askofu Luigi, pamoja na Waziri wa Elimu wa Laikipia Hon. J.B. Akaale, na Laikipia Women Rep. Hon. Jane Apollos, na wageni wengine.

### *PPC, PFC, na Parish Assembly ya 10*

Baada ya shughuli za Harambee na Sherehe za Paska, kutakuwa na mikutano ya *Parish Pastoral Council* (PPC), *Parish Finance Council* (PFC), ili kupanga pia siku ya *'Parish Assembly ya 10'* kwa ajili ya viongozi wote wa Parokia.

### *Semina ya "Junior Catechists"*

Masomo ya *Junior Catechists* yalianza na Semina ya 1 Ijumaa 28 na Jumamosi 29 Machi. Masomo haya ni kuhusu jinsi ya kulihudumia Kanisa kama Makatekista. Waliojiandikisha ni watu 18. Masomo haya yataendelea karibu kila mwezi: Semina ijayo itakuwa Ijumaa 2 na Jumamosi 3 Mei. Semina hizi zinapangwa na Kamati ya Makatekista (bw. Francis Wambugu na bw. John Ndungu).

### *Miche inauzwa kwenye "Green Ol Moran"*

*Wakulima wa Shamba la Parokia "Green Ol Moran" watangaza kwamba miche ya miti ya bustani na miti ya matunda iko tayari kuuzwa. Miti ya matunda inayopatikana hasa ni maembe, avocado na matunda damu.*

### *Scout Group Ol Moran 1: In-Take 2014*

Maskauti wa Parokia wanatangaza nafasi ya kujiandikisha katika chama chao. Katika kituo cha *'Mwamba Scouts'* huweza kujiandikisha wasichana na wavulana wa kidato cha 1, 2 na 3. Siku ya mwisho ni Jumapili 30 Machi. Wanaotaka kujiunga nao waongee na Mr. Anthony Nguni au Mr. David Munyiri, au Fr. Giacomo. Watakutana mara ya kwanza Jumapili 6 Aprili.

Bali kituo cha *'Rovers'* ni cha vijana baada ya Shule ya Upili. Hawa wanaendelea na kazi zao mbalimbali. Wanaotaka kujaribu njia yao, huweza kujiunga nao wakati wowote.

Ni mpango wa kikundi cha Maskauti kufungua kituo cha watoto wadogo pia (Sungura na Chipukizi Scouts), katika Shule ya Msingi ya Tumaini, muhula ujao.



*Nyahururu, Jumamosi 22 Machi 2014*

# Sherehe ya Jimbo

Katika Ibada ya Jumamosi 22 Machi 2014, Jimbo la Nyahururu lilipata sababu kadhaa ya kusherehekea na kumshukuru Mungu.

- Ibada ya Kuwekwa Wakfu kwa Mapadri wapya 6, na Mashemasi 3 wa Jimbo la Nyahururu;
- Siku ya kutimiza miaka 11 ya Jimbo la Nyahururu;
- Miaka 11 ya Uaskofu wa Askofu Luigi Paiaro;
- Miaka 25 ya Upadrisho na 2 ya Uaskofu wa Askofu Joseph;
- Kufungua rasmi Mwaka wa Familia katika Jimbo la Nyahururu.

Ibada ya Misa iliyoongozwa na Baba Askofu Joseph Mbatia, kuanzia saa nne, Tabor Hill, akiwa pamoja na Askofu Mstaafu Luigi, Vicar General Fr. Stanley Wambugu, na Mapadri wa Jimbo la Nyahururu na majimbo mengine pia. Wakristu wengi walikuja kuhudhuria ibada na kushuhudia yaliyotendwa siku hiyo.

Baada ya Hotuba yake, Askofu aliendelea na ibada ya Ushemasi na Upadrisho. Halafu, kabla ya baraka ya kumalizia Misa, alizibariki familia kadhaa zilizoakilisha familia zote za Nyahururu, na kwa njia hii kufungua rasmi Mwaka wa Familia jimboni mwetu.

Mashemasi wapya 3:

- Deacon Kennedy Mwaura (kuzaliwa 1986; kutoka Manunga Parish);
- Deacon Nicholas Kiboi (1984; Sipili Parish);
- Deacon Paul Gacheke (1983; Magumu Parish).

Mapadri wapya 6:

- Rev. Fr. David Githinji (kuzaliwa 1977; kutoka Murungaru Parish);
- Rev. Fr. Samuel Wainaina (1983; Magumu Parish);
- Rev. Fr. Fredrick Mwangi (1982; Magumu Parish);
- Rev. Fr. Paul Ngure (1978; Geta Parish);
- Rev. Fr. Paul Munyaga (1983; Ol Kalou Parish);
- Rev. Fr. James Mathenge (1984; Ngorika Parish).

### Parokia mpya ya Shamanei

Jimbo Katoliki la Nyahururu laongeza Parokia mpya, kule Shamanei (kutoka Nyahururu kuelekea Nakuru).

Askofu Jospeh aliifungua Jumamosi 29 Machi asubuhi, akimkabidhi Fr. John Gakena jukumu la kuliongoza kama Baba Paroko wa kwanza. Hiyo itakuwa Parokia ya 32 ya Jimbo.

*Mwisho wa Muhula wa 1 wa mwaka 2014*

## Majuma ya likizo na Muhula wa 2

Shule zinaelekea kufunga muhula wa 1 wa mwaka huu, na wanafunzi kurudi nyumbani. Muhula wa kwanza utafungwa Alhamisi 10 na Ijumaa 11 Aprili. Wanafunzi watabaki nyumbani kwa muda ya majuma 3.

Hekima House itafungua muhula wa 2 Jumatatu jioni 5 Mei, ili wanafunzi waingie darasani tena Jumanne asubuhi 6 Mei.

Watoto wa Tumaini Academy wataanza muhula wa 2 wakiingia darasani Jumatatu 5 Mei asubuhi kama kawaida.

### *Miti ya SSP*

Mvua ikirudi, hata mradi wa SSP wa kupanda miti unaanza tena. Miti itapandwa na Wanafunzi wanaofadhiliwa na SSP, pia na wanafunzi wote wa Hekima House. Kila mwanafunzi ana jukumu la kupanda miti 5, kila muhula.

Wataanza wanafunzi wa Hekima House kupanda miti katika shamba la shule ya Tumaini. Wanafunzi wa Hekima ni 96, kwa hivyo itapandwa miti 480. Wanafunzi wengine wa Shule za Upili za Ol Moran na Mithuri watajulishwa baadaye kuhusu mpango wao.

### *Hekima Day 2014: Jumamosi 17 Mei*

Sherehe ya Hekima House ya mwaka 2014 itakuwa Jumamosi tarehe 17 Mei. Katika sherehe hiyo, inayofanywa kila mwaka, wanaalikwa hasa wazazi wa wanafunzi, pia wanafunzi waliosoma Hekima miaka iliyopita na wakatoka.

Sherehe itaanza na Misa saa nne, kisha itaendelea na mkutano wa Wazazi, chakula cha mchana na ngoma.

### *Tumaini Academy imepata Registration*

Baada ya mwaka mmoja wa kujaribia mpango wa shule ya msingi wa Parokia, Tumaini Academy imepata "*Registration*", yaani kitambulisho kilicho ruhusa ya Serikali ya Kenya ya kufanya masomo na mitihani ya shule.

### Kazi ya kutengeneza barabara

Ahadi zimetimizwa, lakini bado kamili. Barabara nyingi katika Wards za Ol Moran na Sosian zilitengenezwa miezi iliyopita. *Graders* mbili zilizotumwa na Serikali ya Kaunti zilifanya kazi kwa siku kadhaa katika vijiji vyetu, halafu zilirudishwa Nanyuki. Juzi zilirudi na kuanza kufanya kazi tena.

Hayo yote ni kazi njema. Hata hivyo, wasiwasi kuhusu hali ya barabara imebaki, hasa kwa sababu ya barabara kuu Sipili-Ol Moran. Kwa kweli ilikuwa imesemwa kwamba *murram* itatandazwa hasa kwenye sehemu mbaya, hata juu ya barabara kuu, lakini kazi hiyo haijafanywa na sasa mvua imeanza kufika. Bila mchanga mgumu kuna uwezekano kwamba kazi nyingi zitapotea bure na barabara zitaharibika haraka.

### Mkasa wa moto Laikipia Nature Conservancy

Hasara kubwa katika mazingira ya Laikipia Nature Conservancy ilisababishwa na mkasa wa moto ulioanza Jumapili 9 Machi na kuendelea siku kadhaa, ukiharibu ekari yapata elfu 50. Kulingana na uchunguzi wa Conservancy, moto uliakishwa kwenye sehemu mbalimbali na wahalifu wanaotaka kudhuru kazi ya kuhifadhi mazingira na wanyama wa porini.

*Maendeleo katika eneo letu*

## Booster ya Simu: Network iko!

*Matarajio ya wenyeji wa Ol Moran na vijiji jirani yalikuwa makubwa, wakiona Booster ikijengwa kijijini kwao. Na kuanzia Jumamosi 29 Machi ilianza kufanya kazi.*

*Mtandao wa simu wa Kampuni ya Safaricom utasaidia sana mawasiliano ambayo yamekuwa changamoto kubwa kwa miaka mingi katika eneo letu, hasa katika shida ya usalama na wizi, lakini pia kwa biashara na kazi nyingi.*

*Sasa simu zimejaa Network! Lakini Wakristu wajue kuizima simu wakifika kanisani: ikilia itasumbua, na bila shaka haiwezi kuwa "Call" ya Mungu!!*

